MANISPAA

KATIKA makala ya "Asemavyo Mhariri" yaliyotokea wiki iliyopita katika gazeti hili letu tukufu la *COASTWEEK*, nime furahika sana kuona Mhariri amekumbusha Baraza la Manispaa juu ya umuhimu wa kuuweka mji wetu katika hali ya usafi.

Nikizidi kusisitiza juu ya uchafu ulioko Mombasa, napenda kumkumbusha. Mhariri kwamba si Mwembe Tanganyika pekee ambapo uchafu hubaki kwa kipindi kirefu, bali hata sehemu nyingine za mji huu kama Spaki, Mvita, Mwembe Tayari sokoni na sehemu kadha nyingine.

Kwa hivyo, Baraza la Manispaa ya Mombasa lina jukumu kubwa la kuona mji wetu huu uliokuwa msafi na ukisifika katika Afrika Mashariki kama ulio msafi kuliko yote. utawekwa katika hali ya kuridhisha.

MBARAK SALIM (KD)
MOMBASA.

WAALIMU

NIKIWA mzazi ambaye nina watoto wanaosoma katika shule mojawapo hapa Mombasa, ninapenda kuwaomba waalimu wafanye bidii kuwafunza wanafunzi ili wafaulu kwenye mitihani yao.

Wakati watoto wangu ambao kwa wakati huu wako likozoni kwa kuwa shule zimemaliza kipindi cha kwanza, nilijaribu kuwafanyia majaribio kadha yanayohusiana na elimu ya madarasa waliyokolakini kwa mshangao, hawakuweza kuyajibu.

Ingawa watoto wangu wanapofika nyumbani wanaonyesha bidii kubwa ya kutalii, lakini udhoofu nina uhakika unatokana na mafunzo yasiyoridhisha ya waalimu wao. Mtoto asiye na bidii huonyesha wazi lakini mwenye bidii dalili yake inaonekana kwa kutalii akiwa nyumbani.

Natoa ombi kwa waalimu wazidishe bidii kuwafunza wanafunzi masomo yanyotakikana na yaliyo muhimu kwa watoto kuyajua.

Mohammed Mussa.
MOMBASA.

WITO KWA FEISAL FC: FANYENI BIDII SANA

KAMA MPENDA soka ambaye sipendi kukosa kuangalia michuano ya mchezo huo katika Stadium ya Mombasa, nimependezwa na vile ile timu ya Feisal FC inavyoligota kabumbu la hali ya juu na nawaomba wachezaji wazidishe bidii ili mwakani wacheze Supaligi.

Feisal FC timu iliyokuwa maarufu nyakati za *"kale"*, imeanza vyema katika Ligi ya Wilaya ya Mombasa ambayo ina timu kadha maarufu zinazoshiriki na bila shaka Feisal itakuwa mojawapo ya zile zitakazomaliza mstari wa mbele.

Lakini natoa ombi kwa wachezaji washikilie kamba ile ile ya *"kurudi nyuma mwiko"* - ili izidi kujinyakulia pointi nyingi na ifikapo mwaka 1985, irudi katika Ligi ya Taifa na irudishe hadhi yake iliyokuwa nayo miaka ya nyuma hasa kipindi cha miaka ya 60.

Namaliza kwa kutoa ombi kwa Viongozi wa klabu hiyo ya Feisal, wazidi kuwapa nguvu wachezaji wafanikiwe katika lengo ambalo sisi mashabiki wa klabu hiyo tunahamu nalo; na lengo lenyewe ni kuona timu yetu imefikia kiwago cha kustahili kurudi Supaligi.

Heko Feisal, daima twende mbele na tuweke mioyoni mwetu kwamba kurudi nyuma ni mwiko!

ABDUL-LATIF OMAR
Mji wa Kale.
MOMBASA.

UNAPOPATA mtoto wakati wa sikukuu yoyote huwa furaha zaidi. Na baadhi ya waliojaaliwa kujifungua mtoto wakati wa Pasaka si mwingine ila ni mke wa Assistant Administrative Office Manager, wa Kampuni ya BAT, Bw. Julius Oduor Enson. Bibi Dorcas anaonekana na mtoto wake akiwa pamoja na Siser Juma (kushoto) na Nurse Mary Mguyi (wa Aga Khan Hospital) na Mama Rahabu. PICHA: CAESAR MADDANGANHA

BINT EL SUDAN
Perfume * Powder
Pomade * Deodorant
DEODORANT SPRAY YA MARASHI ASILI YA MAPENZI
HAKIKA UTA FURAHI

Wasiliana Na KFF Pwani - Asema Meya Mwidani

VILABU VYA Soka wilayani Mombasa vimeombwa viwasilishe matatizo yao kwa Shirikisho la Soka (KFF) na vikatakiwa kuepukana kujiingiza kwenye mambo ya siasa kwani vikifanya hivyo, kutazorotesha maendeleo na pia huenda vikajikuta vinamalizika kabisa.

Ombi hilo lilitolewa na Meya wa Mombasa, Diw. Ahmed Mwidani wakati alipohutubia viongozi wa vilabu Vya Soka Vya Mombasa katika Ukumbi wa Tononoka kwenye sherehe za kutoa vikombe kwa vilabu vilivyoshinda mwaka uliopita wa 1983.

Diw. Mwidani alisema hali ya mchezo wa kandanda katika Mombasa imekuwa ya kusikitisha ukilinganisha na miaka michache ya nyuma ambapo wachezaji kadha walikuwa wakiliwakilisha Taifa kwenye michuano ya Kimataifa.

"Kutokana na hali hiyo", Diw. Mwidani alisema na kuongeza, "ni juu ya KFF kutayarisha semina kwa vilabu vyetu vipate mafunzo ya mbinu za kisasa za kulisakata soka. Nina uhakika semina zikifanyika, hali ya mchezo itabadilika na kuwa kama miaka iliyopita"

Diw. Mwidani alisema Baraza la Manispaa ya Mombasa na KFF Pwani itakuwa ikikutana mara moja kila mwezi kutatua matatizo na kujadiliana juu ya ufumbuzi wa matatitzo hayo. "Hapana haja ya kukimbilia magazetini kwani mikutano kama hii ndiyo pekee yatakayofumbua matatizo na kuvarekebisha" akaongeza Baba wa Mji wa Mombasa.

Katika hafla nyingine ya Harambee ya kuchangia klabu ya Harambee, Diw. Mwidani aliviomba vilabu vya starehe na michezo vishirikiane kwa mafanikio mema.

Alikisifu klabu cha Harambee kwa kutimiza zaidi ya miaka ishirini na akaongeza, "mafanikio yenu yametokana na ushiriki ushirikiano na maongozi mazuri, na nawaomba mudumishe mwenendo huo"

"Nina majivuno kusema kwamba klabu hichi cha Harambee kimekuwa na matendo na maongozi yanayoambatana kikamilifu na ujenzi wa taifa hili kama kuwalipia karo wanafunzi walio na jamii masikini na kuchangia mipango mbali mbali ya maendeleo ya mji huu na Kenya kwa ujumla", akasifu.

Diw. Mwidani aliye Mwakilishi wa sehemu ya Port Reitz alitoa ombi kwa wakazi wote wa Mombasa na kwengineko, makampuni na mashirika wajitokeze kukisaidia kilabu hicho ili kiweze kuendesha shughuli zake za ujenzi wa taifa.

MCHANGO

Diw. Mwidani Alitoa mchango wake wa 1,852/-. Madiwani na viongozi kadha walihudhuria tafrija hiyo iliyofanyika katika makao makuu ya klabu hicho kuko Bondeni, Mombasa

Madaraka Ya Juu Kwa Andy Nyaga

TAWI LA PWANI la Maonyesho ya Ukulima (ASK) linafanya taratibu la kuwajengea wafanyakazi wake nyumba. Mwenyekiti wa tawi hilo, Bw. Brown Ondego alisema.

Akizungumza na Mwenyekiti Mwenezi wa mwaka huu wa Maonyesho, Bw. Andy Nyaga, Bw. Ondego alisema mkutano mkubwa wa Harambee wa kuchangia mpango huo utafanyika hivi karibuni.

Bw. Nyaga aliye pia mstiikiliaji wa muda wa cheo cha Afisa Mwenezi wa Kampuni ya Kenya Cargo Handling Services Limited alipewa wadhifa wa kuwa Mwenyekiti Mwenezi wa ASK tawi la Pwani.

Kabla ya kujiunga na kampuni ya K.C.H.S., Bw. Nyaga alikuwa mwandishi wa gazeti la kila

• *BW. NYAGA*

siku la *"The Standard"* katika afisi ya Mombasa. Ni kijana mwenye bidii na ni mategemeo makubwa atatekeleza kazi yake hiyo mpya kwa uwezo alio nao.

MSIBA MKUBWA

BI. NDELIMIKO Johana Mbele (pichani), mke wa Padri wa Kwanza Taveta, aliaga dunia hivi majuzi akiwa na umri wa miaka 90. Mamia ya waombolezi wakiwemo watoto wake sita na wajukuu zaidi ya 40 walihudhuria mazishi yake yaliyofanyika Taveta Mlimani, nyumbani kwake. Marehemu alikuwa Mkristo aliyejishirikisha kikamilifu katika mambo ya dini yake na pia alikuwa mkulima stadi. Marehemu alikuwa mama yake Bi. Rechel Mzera, Senior Administrative Programmer na Shirka la Umoja wa mataifa (UNDP), Nairobi. Mmoja wa wajukuu wake ni Mwandishi Maarufu wa *COASTWEEK* Bw. Gray Phombeah.

• *BI MBELE*

ASEMAVYO MHARIRI

KWA kipindi kikubwa sasa, Kenya ni mojawapo ya nchi ambazo zimejitegemea sana katika utoaji wa chakula cha kutosha kwa wananchi wake na hii imetokana na bidii ya wakulima wetu.

Kipindi cha mvua kote nchini kimeanza na huu bila shaka ni wakati mzuri kwa wakulima wetu kuuchukulia katika kulima bidhaa kadha muhimu hasa zile ambazo ni vyakula tunavyotumia.

Tunamshukuru Mwenye-ezi-Mungu kwa kutujaalia kuwa na ardhi yenye rutba nzuri ambayo imetufanya tujitegemee sana kwa chakula chetu cha kila siku.

Hakika Wapwani hatuna budi kufunga mikanda yetu barabara ili tuanze kulima kwa wakati huu ambapo Mwenyeezi-Mungu ametujaalia mvua ya kutosha. Bila shaka wakulima watachukulia wakati huu kwa kutekeleza kazi zao.

Kwa wakazi wa mijini ambao wako likizoni makazini mwao, hawana budi kusafiri hadi nyumbani mashambani ili kusaidia jamaa na ndugu katika kulima na Kenya yetu izidi kunawiri na kujitegemea.

Umoja ni nguvu! hatuna budi kushirikiana kulijenga taifa letu. Tuitikie mwito wa Mtukufu Rais Wetu Mpendwa, Daniel arap Moi wa kwenda 'kasi' katika shughuli za maendeleo.

Farucci

BINT EL SUDAN
Perfume * Powder
Pomade * Deodorant

MARASHI ASILI YA MAPENZI
HAKIKA UTA FURAHI

JISHINDIE VIATU MARIDADI VYA FARUCCI KWA MSHINDI WA KWANZA NA 'BINT EL SUDAN - GIFT PACK' KWA WASHINDI WA PILI NA WATATU KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO

CROSSWORD No. 185

KWENDA CHINI: 1. Nitunda kisha mji wa Kenya. 2. Aina ya maua. 3. Makab ya Rais. 4. Mtu anayetembelea nchi na kujionea mambo mbali-mbali. 10. Tapia, kimbilia. 12. Zuia utesi. 14. Pande la chombo kilichovunjika. 15. Maoni, shauri. 17. Tamko la kukataa. 18. Kinyume

KWENDA KULIA: 1. Kifua cha kuku. 5. Jani la mnazi. 6. Mtoto wa nzige. 7. Kito cha.thamani. 8. Kamilika, tosha. 9. Afrika Mashariki. 11 Pamoja na. 13. Nguruwe mwitu. 16. Moyo. 17. Kama. 19. Ae kama ilivyo. 20. Pinda mgongo ukielekea chini.

Majibu ya shindano la Fumbo la Kujaza Maneno No. 184. *Kwenda Kulia:* 1. UKAMBAA, 5. HAMALI, 6. AM, 8. ZA, 9. MBUI, 10 PA, 11. GAWA, 12. UMA, 13. ANGUA, 15. ONI, 16. NA, 17. TAA, 18. SINIA. *KWENDA CHINI,* 1. UCHUNGU, 2. MWAMBANI, 3. AJIZI, 4. JA, 7. MGAAGAA, 9. MWANA, 10. PM. 12. UA, 14. UTI, 15. OA, 16. NI.

Washindi waombwa wafike a''sini mwa COASTWEEK.

WASHINDI WA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 184.

1. Hasira N. Wanje, Sanduku La Posta 86046, Mombasa, 2. Peter W. Mpwipwipo, Sanduku La Posta 90404, Mombasa. 3. Izaca Salim, Sanduku La Posta 93940, Mombasa.



JINA..........................

SANDUKU LA POSTA....................

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yetakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata viatu na 'Bint El Sudan - Gift Pack'. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK* limited Mombasa. Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Mhariri *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya jumatano tarehe **May 2. 1984** saa, nne asubihi shindano hili litakuwa mwisho.